Washington State Department of Social & Health Services

# Mpango wa Wajibu Binafsi (IRP)

Mpango wa Wajibu Binafsi wa WorkFirst kwa ____________________________

| Kitambulisho cha JAS | NAMBARI YA KESI |
|---|---|
| KITAMBULISHO CHA MTEJA | |

Ninaelewa kwamba:

- Ninahitajika kufanya kazi, kutafuta kazi na kujitayarisha kwa kazi.
- Lazima nishiriki katika shughuli zinazohitajika. Iwapo sitashiriki, nitaadhibiwa isipokuwa kama nina sababu mwafaka. Hii inarejelewa kuwa katika hali ya vikwazo vya WorkFirst.
  - Iwapo nimewekewa vikwazo, hii inamaanisha:
    - Ruzuku yangu itapunguzwa kwa 40% au sehemu ya mtu mmoja, ikitegemea ni ipi kubwa, AU:
    - Sitaweza kupokea huduma za usaidizi, isipokuwa nitashirikiana upya na WorkFirst.
  - Iwapo msaada wangu wa fedha utapunguzwa kutokana na vikwazo vya WorkFirst:
    - Huenda nikahitajika kufuata IRP yangu kwa wiki nne mfululizo ili kuondoa vikwazo.
    - Mara ninapokidhi masharti kwa wiki nne mfululizo, adhabu yangu ya vikwazo itakwisha kuanzia mwanzo wa mwezi baada ya wiki nne za ushiriki wangu.
    - Kesi yangu itafungwa iwapo nitaendelea kuwa na vikwazo kwa miezi kumi mfululizo.
  - Iwapo kesi yangu itafungwa kutokana na vikwazo vya WorkFirst:
    - Nitahitajika kutuma ombi upya na huenda nikahitajika kushiriki kwa miezi minne mfululizo kabla niweze kupokea fedha.
- Lazima nishirikiane na Kitengo cha Usaidizi wa Watoto wakati ninapokea msaada wa TANF/SFA isipokuwa kama nina sababu mwafaka ya kutoshirikiana. Ukusanyaji wa msaada wa watoto unaweza kuondoa hitaji langu la usaidizi wa fedha.
- Ninaweza kupata miezi 60 pekee ya misaada ya fedha ya TANF/SFA katika maisha yangu isipokuwa kama ninastahiki nyongeza.
- Nimetumia miezi _____ ya msaada wa fedha.
- Ninahitajika kufanya kazi, kutafuta kazi na kujitayarisha kwa kazi. Iwapo nitashindwa kuhudhuria shughuli iliyoratibiwa, nitampigia simu mtu kwenye nambari iliyoorodheshwa hapo chini.
- Lazima nifanye shughuli zifuatazo kwa kiwango cha saa kila wiki kilichobainishwa hapo chini:

Iwapo nina sababu mwafaka ya kutofuata mpango wangu, lazima niwasiliane na nishirikiane na Wataalamu/Wafanyakazi wa Jamii wa Mpango wa WorkFirst haraka iwezekanavyo. Baadhi ya mifano ya sababu mwafaka ni pamoja na:

- Nilikosa kuhudhuria miadi kutokana na maradhi au tatizo lisilotarajiwa kwenye huduma ya utunzaji wa mtoto wangu au usafiri;
- Nina hali ya dharura (kimwili, kiakili au kihisia);
- Mimi ni mwathiriwa wa dhuluma ya kinyumbani;
- Nimeshindwa kupata huduma ya utunzaji wa watoto ambayo ninaweza kumudu na inayofaa katika eneo langu kwa watu walio na umri wa chini ya miaka 13;
- Nina tatizo lililopo la kisheria;
- Nina ulemavu au matatizo fulani na hali hii imenifanya nishindwe kukidhi masharti ya mpango; au
- Mimi ni mtu mzima aliye na ulemavu mkubwa na sugu;
- Ninahitajika nyumbani ili kumtunza mtoto wangu aliye na mahitaji maalum au mtu mwingine mzima aliye na ulemavu;
- Nina umri wa miaka 55 au zaidi na ninamtunza mtoto ambaye mimi sio mzazi wake; au
- Ninaomba SSI kupitia mwezeshaji wa DSHS.
- Sina makazi au natunza mtoto (watoto) wasio na makazi.

Iwapo sikubaliani na mpango huu, nina haki ya kuomba ukaguzi wa kesi na/au Usikilizaji wa Kesi ya Usimamizi. Ili kuomba usikilizwaji wa kesi, ni lazima niwasiliane na Ofisi ya Huduma za Jamii au Ofisi ya Usikilizwaji wa Kesi ya Usimamizi ya eneo langu, DSHS, PO Box 42489, Olympia WA 98504-2489, ndani ya siku 90 kutoka tarehe ya saini ya msimamizi wa kesi yangu hapo chini. Nimepewa nakala ya Mpango wangu wa Wajibu Binafsi. Wakati wa usikilizwaji wa kesi, nina haki ya kujiwakilisha, kuwakilishwa na mwanasheria au mtu yeyote mwingine ninayechagua. Ninaweza kupata ushauri wa kisheria au uwakilishi wa bila malipo kwa kuwasiliana na huduma ya Ushauri na Rufaa Iliyoratibiwa ya Elimu ya Kisheria (CLEAR) kwa:

- Kutembelea tovuti yake http://nwjustice.org/get-legal-help;
- Kupiga simu 1-888-201-1014 iwapo ni umri wa chini ya miaka 60, au
- Kupiga simu 1-888-387-7111 iwapo ni umri wa miaka 60 au zaidi.

| SAINI YA MSIMAMIZI WA KESI | TAREHE | SAINI YANGU | TAREHE |
|---|---|---|---|
| | | | |

| Kitambulisho cha JAS | NAMBARI YA KESI | KITAMBULISHO CHA MTEJA |
|---|---|---|
| | | |

## MASHARTI YA SIRI

Ninaweza kupokea huduma za usaidizi ili kunisaidia kuendeleza kazi yangu, kudumisha kazi yangu, kukubali kazi, kutafuta kazi au kufuata mpango wangu. Iwapo sitakubaliana na uamuzi kuhusu huduma za usaidizi, ninaweza kuomba ukaguzi wa kesi na/au usilikizaji wa kesi. Nitawasiliana na Mtaalamu/Mfanyakazi wa Jamii wa Mpango wa WorkFirst iwapo ninahitaji huduma za usaidizi kama vile:

- Matengenezo ya gari
- Mavazi
- Ushauri nasaha
- Nepi
- Kulipia gharama za elimu
- Usafi wa kibinafsi
- Kulipia leseni/ada
- Kunyoa nywele
- Pasi za basi
- Mafuta ya gari
- Zana za kazi
- Kupanga uzazi

Wakati wa vikwazo, siwezi kupata huduma za usaidizi (kama vile pesa za kununua mavazi ya kazi au usafiri) hadi nitakapoanza kufuata IRP yangu.

Ninaelewa kwamba, iwapo nitakataa kushirikiana na Kitengo cha Usaidizi wa Watoto (DCS) bila sabau mwafaka, huenda ruzuku yangu ikapunguzwa. Sababu mwafaka zinajumuisha tishio la madhara kwa watoto wangu au mimi. Ninaelewa kuwa wakati ninapata msaada wa TANF, msaada wowote wa watoto unaokusanywa huzuiliwa ili kulipa jimbo.

Nitakapoacha kupata TANF/SFA, DCS itakusanya msaada wa watoto na kuutuma kwangu isipokuwa nitawaomba waache. Ninaelewa kuhusu huduma za usaidizi, vikwazo na msaada wa watoto.

| SAINI YA MSIMAMIZI WA KESI | TAREHE | SAINI YANGU | TAREHE |
|---|---|---|---|
| | | | |